


Je, Tunaishi Katika “Siku za Mwisho”? (Sehemu ya 1)

Inategemea sura ya 9 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye tovuti ya jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, HIZI NI “SIKU ZA MWISHO”?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Huenda watu wengine wakasema nini?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA BIBLIA INASEMA NINI

Neno la Mungu lilitabiri kuhusu kipindi kinachoitwa siku za mwisho.

(Tazama sura ya 9 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 1 hadi 5.)

Soma Isaya 46:10.

Kwa nini tunaamini kwamba Yehova ana uwezo wa kutabiri kuhusu siku za mwisho?

Soma Mathayo 24:3 na 2 Timotheo 3:1.

Mistari hii inaonyeshaje kwamba mfumo wa mambo wa sasa wa wanadamu utakoma?



Kama vile alama zinavyoweza kukusaidia ujue ikiwa umekaribia mahali unapokwenda, hali za ulimwengu zinathibitisha kwamba tumekaribia mwisho wa mfumo huu wa mambo

Neno la Mungu lilitabiri kuhusu nyakati tunazoishi.

(Tazama sura ya 9 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 6 hadi 11.)

Soma Mathayo 24:7 na Luka 21:11.

Ni mambo gani yanayotajwa katika mistari hii ambayo wewe binafsi umeona au umesikia?

Soma 2 Timotheo 3:1-5.

Umeona watu wakionyesha tabia gani mbaya kati ya hizi?

Ni nini kinachokusadikisha kwamba tunaishi katika siku za mwisho?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

Sikuzote kumekuwa na vita, njaa, na majanga ya asili. Hivyo hakuna jambo la pekee kuhusiana na wakati wetu katika historia.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Ni kweli kwamba mambo haya yamekuwapo kwa miaka mingi sana. Lakini ninaamini kwamba wakati wetu *ni* wa pekee kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?

MTU AKISEMA . . .

Huenda unabii huo utatimia katika kipindi fulani cha wakati ujao.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Labda watu wengi watakubaliana na maoni yako. Lakini ninaamini jambo tofauti kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?
